# MTIHANI WA DARASA LA SITA
# MUHULA WA PILI-2018

*Muda: Saa 1 dak 40*

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.**

__1__ serikali __2__ uchomaji makaa miaka __3__ iliyopita __4__ la ajabu ni kuwa __5__ ya makaa __6__ kuongezeka mwaka __7__ mwaka. Takribani __8__ sabini ya kawi inayotumiwa kila mwaka __9__ Kenya inatokana na __10__.

1. A. Lakini B. Angalau C. Ingawa D. Aghalabu
2. A. haikupiga marufuku B. ilipiga marufuku C. ilihalalisha D. haikuharamisha
3. A. kadhaa B. kadha C. kadhaa wa kadhaa D. mbili
4. A. mambo B. neno C. hali D. jambo
5. A. maonyesho B. matumizi C. maangamizi D. utumiaji
6. A. imezidi B. hayajazidi C. yanazidi D. yatazidi
7. A. baada ya B. kabla ya C. badala ya D. pamoja ya
8. A. idadi B. asili C. asilia D. asilimia
9. A. inchini B. kwa taifa la C. nchi ya D. nchini
10. A. makaa B. miti C. kuni D. mbao

Ilikuwa __11__ kuwa siku hiyo __12__ mtihani wa mwigo. Ikanibidi __13__ vilivyo kwani sikutaka __14__ __15__ wa matokeo.

11. A. dhahiri shairi B. thahiri shahiri C. dhahiri shahiri D. dhahiri shayiri
12. A. tutafanya B. tungefanya C. tunafanya D. tulifanya
13. A. kujiandaa B. kuandaa C. kuandalia D. kujianda
14. A. kufedheheka B. kufadhaika C. kusifika D. kupongeza
15. A. saa B. wadhifa C. wakati D. waadhi

**<u>Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa.</u>**

**16.** Fura ni kwa hamira kama vile baidika ni kwa ________.

A. wali wa daku
B. kifaranga aliyenyeshewa na mvua
C. mwana aliyezaliwa Ijumaa
D. ardhi na mbingu

**17.** Makao ya kuku ni

A. kizimba
B. kombe
C. zizi
D. mzinga

**18.** Usemi wa taarifa wa "Hakuna mtoto wangu atakayeteseka sasa," Baba alisema, ni

A. Baba alisema kuwa hakuna mtoto wake angeteseka sasa
B. Baba alisema kuwa hakuna mtoto wake atakayeteseka sasa
C. Baba alisema kuwa hakuna mtoto wake ambaye angeteseka wakati huo
D. Baba alisema kuwa hakuna mtoto wake atateseka wakati huo

**19. Tegua kitendawili:** Abeba mishale kila aendako

A. Nungunungu B. Chui
C. Nyuki D. Kuku

**20.** Chagua msamiati wa riadha pekee

A. Kukimbia, kuogelea, kwata, jugwe
B. Kukimbia, kuogelea, jugwe, miereka
C. Kukimba, kuruka, miereka, kambumbu
D. Kukimbia, gori, kwata, masumbwi

**21. Neno wasichana katika sentensi hii limetumika kama:**

Wanafunzi wasichana wanatia fora:

A. kivumishi rejeshi
B. kivumishi sifa
C. kivumisha jina
D. kivumishi halisi

**22.** Samaki hawa walivuliwa jana. Sasa wananuka

A. shombo B. hombo
C. sombo D. yombo

**23.** Nomino kutokana na kitenzi **amka** ni

A. uamuzi B. mwamko
C. mwamuzi D. umuka

**24.** Nahau - '**kupiga hatua**' ina maana:

A. kutembea B. kuamua
C. kuendelea D. kuadhibu

**25.** Kamilisha methali: Mwiba wa kujidunga ____

A. huwa hauonekani
B. hauna kilio
C. hauumizi sana
D. hauambiwi pole

**26.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi cha nafsi

A. Yeye akichaguliwa ataongoza vizuri
B. Mwenyewe alipofika aliwalipa walinzi
C. Pale alipokomea mwenyeji, mgeni komea hapo
D. Mvumilivu ndiye alaye mbivu

**27.** Mswaki ni wa kusugulia meno kama vile _____ ni kwa kulainisha mbao.

A. msasa B. tupa
C. upawa D. utepe

**28.** Neno **vipepeo** liko katika ngeli gani?

A. A-WA B. KI-VI
C. U-I D. I-ZI

**29.** Maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hii yana maana gani?

Wanafunzi wameanza <u>kukipigia debe</u> Kiswahili.

A. wanakitangaza B. wanakipuliza
C. wanakichunguza D. wanakitukuza

**30.** Chombo ni kwa vyombo kama vile karatasi ni kwa

A. makaratasi B. vikaratasi
C. mikaratasi D. karatasi

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 31 - 40**

Ulimwengu huu wa walimwengu umejaa uozo na uchafu wa kila aina. Mazingira machafu, mitaa michafu, vitendo vichafu, watu wachafu na hata fikra zao chafu. Pote, kote na mote mwavunda, mnuko unaozidi ule wa kilihafu. Je, wapi maadili na nyaadhi za wakuu na makungwi zilizowahi kutiliwa maanani? Kwa nini hata wazazi huwapotosha vijana kwa mavazi yao machafu?

Kwa nadhari zangu, naamini wakuu wetu wamewatelekeza vijana kamasi kuyaambaa majukumu yao. Awali, wazazi walikuwa dira ya jamii. Waliwaelekeza vijana wote wa jamii bila ubaguzi. Lo! Hayo hayapo tena siku hizi. Je, tangu lini mkono mmoja ukamlea mwana?

Ufikapo mijini, utayaona maajabu ya Musa. Usiajibie miondoko ya mavazi ya kisasa kabla ya kushangazwa na michafuko ya madanguroni na vilabuni mwa kubugia vileo. Waraibu wa mivinyo hawaoni haya kudengua viuno wakiwa nusu uchi. **Miiko** haipo tena. Ole wao waliotupia mbwa hadhi na utukufu na kusazwa na unyama! Sasa mja na hayawani ni sawa bin sawa. Kuvaa nguo na kubaki rabana yote ni mamoja. Nashangaa.

Je, umewahi kuitembelea mitaa ya mabanda? Huko kumejaa vijana wa mitaa, mabiwi ya taka, majitaka na hata mmomonyoko wa maadili. Kuko huko ndiko utakako [illegible]a visa vya kutamausha kama vile: ubakaji, mauaji ya kinyama au mikurupuko ya magonjwa sugu.

Wakati umefika, tuchukue hatua. Tuwe katika mstari wa mbele ili tuitakase hadhi ya mwanadamu. Tuamke sote, tupige hatua iwapo hatutaki kuangamia.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, si kweli kusema kuwa
- A. mazingira ndiyo machafu tu
- B. ulimwengu hauvutii kama zamani
- C. zamani wazee walizoea kuwashauri vijana
- D. wazazi pia huvaa mavazi yasiyo ya heshima

**32.** Huenda uozo huu katika jamii umezidishwa na:
- A. utajiri mijini
- B. ukosefu wa elimu
- C. ukosefu wa ushirikiano wa wadau
- D. tabia ya vijana kupuuza nasaha

**33.** Neno '**miiko**' katika aya ya tatu lina maana gani?
- A. Vifaa vya kusongea ugali
- B. Tabia nzuri
- C. Tabia ya kushangaza
- D. Mambo yasiyokubaliwa katika jamii

**34.** Vijana wa mitaa hujulikana kwa jina:
- A. vibaka  B. chokoraa
- C. mayatima  D. viokote

**35.** Waraibu wa mivinyo ni wanaopenda
- A. vipawa vyao  B. uraia wao
- C. raha na kazi  D. kunywa vileo

**36.** Wanaotakiwa kufanya juhudi ili kuurudisha ubora wa binadamu ni
- A. maskini
- B. matajiri
- C. wanadamu wenyewe
- D. serikali

**37.** Maneno, '**mabiwi ya taka**' ni fani gani ya lugha?
- A. Nomino ya jamii  B. Misemo
- C. Tashbihi  D. Methali

**38.** Ugonjwa upi hautokani na uchafu?
- A. kipindupindu  B. UKIMWI
- C. Homa ya matumbo  D. Waba

**39.** Mwandishi anawanyoshea wakuu wetu kidole cha lawama kwa:
- A. kutekeleza majukumu yao
- B. kutelekeza wajibu wao
- C. kuwaelekeza vijana ifaavyo
- D. kuhamia majini palipo na mitaa ya mabanda

**40.** Kichwa cha makala haya ni
- A. Miji yenye raha
- B. Vijana wajeuri
- C. Utovu wa maadili
- D. Cha kuvunda hakina ubani

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 41 - 50**

Alipofikishwa mahakamani, Mashaka alijitetea, "Mheshimiwa, nilikuwa nikitoka dukani usiku kama saa tatu hivi. Kulikuwa na giza totoro kwa vile mbingu ilifunikwa na mawingu ya mvua. Mara mbele yangu nikaona macho mawili yaliyong'aa kama nyota. Nikajua bila shaka nimevamiwa na mnyama mkali. Macho yale yakaanza kunikaribia. Nami sikusita. Nikatoa bastola yangu, nikamlenga yule mnyama na kufyatua. Akaanguka na kufa pale pale. Ndipo, kwa mikono iliyokuwa ikitetemeka nikawasha kiberiti changu ili nione alikuwa ni mnyama wa aina gani.

Nilishtuka na kupigwa na butwa nisijue la kufanya nilipoona maiti ya mke wangu - mpenzi imelala mbele yangu!" Enhe yajapo yapokee!

Hakimu akasema, "Kama unayoyasema yangekuwa kweli, ningekuachilia huru kwa vile hukuua mke wako kwa makusudi, bali ulidhani umevamiwa na mnyama mwitu. Lakini yote unayoiambia korti hii ni uongo mtupu." Uongo dhahiri shahiri. Je ni nani angemwamini?

---

**41**. Kulingana na aya ya kwanza
A. Mashaka alikuwa mtuhumiwa wa mauaji
B. hakimu alikuwa amekata kesi
C. usiku huo, palikuwa na mbalamwezi
D. simba alikuwa amemvamia Mashaka

**42**. Kisawe cha **mahakamani** ni
A. kotini
B. jelani
C. katika kituo cha polisi
D. kortini

**43**. Mawingu ya mvua yalisemekana kufanya mbingu kuwa na
A. mvua nyingi
B. upepo mkali
C. kiza kingi
D. kisa kingi

**44**. Kazi ya kiberiti ilikuwa ya
A. kutolea mwangaza
B. kumchomea mnyama aliyeuawa
C. kumshutulia mnyama huyo
D. kufyatulia baruti

**45**. Ni kweli kuwa, hakimu alikuwa
A. mlevi na mvivu
B. jasiri
C. mpumbavu
D. mpenda hongo

**46**. Neno '**mikono**' liko katika ngeli gani?
A. I-ZI
B. U-ZI
C. KI-VI
D. U-I

**47**. Kifaa kilichotumiwa katika mauaji kilikuwa
A. zana ya vita
B. ala ya kufanyia kazi
C. ala ya muziki
D. ala ghushi

**48**. Je, kwa nini hakimu hakumwamini Mashaka?
A. Jamaa huyu alizoea kuua
B. Aliyeuawa alitoa ushuhuda kabla ya kufa
C. Mashaka hakuwa na ithibati tosha
D. Walioshuhudia walimpinga Mashaka

**49**. Maneno '**kupigwa na butwaa**' ni mfano wa:
A. methali
B. msemo
C. tashbihi
D. istiara

**50**. Maudhui yanayojitokeza ni
A. Bastola ni hatari
B. Si vyema kuishi karibu na mbuga
C. Tamaa nyingi haifai
D. Njia ya mwongo ni fupi